The Guardian

Page no 5.



piece –

# *Lack of education cited among reasons for rampant illegal fishing in Tanzania*

By Polycarp Machira, Dodoma

MINISTRY of Livestock and Fisheries has cited lack of education and proper knowledge as one of the reasons why Tanzanian fishermen still engage in illegal fishing.

Responding to a written question by the Special Seats MP, Aida Khenan (Chadema) who had wanted to know if the government was aware why illegal fishing exists in the country asking; "Does the government know why many fishermen engage in illegal fishing despite the efforts to end the menace?" the ministry explained that most fishermen do not understand effects of illegal fishing and use of illegal fishing gear. At the same time, personal behaviour also leads to this without them knowing health and environmental effects of illegal fishing.

The ministry added that the government will continue providing public education on effects of illegal fishing among fishermen in the country, adding that such education has been provided through different forms like radio, television, seminars and other events like Nanenane and World Food Day.

According to the ministry, the government conducted 19 radio programmes, 34 television programmes and several other newspaper articles concerning fishing, environment conservation, among others.

During that period, a total of 43,104 were educated on illegal fishing and improved fishing. At the same time the ministry conducted surveillance in efforts to control illegal fishing, various fishing gear used in illegal fishing.

The ministry said the inspection led to confiscation of 808 illegal fishing equipment and other 149,071 metres of nets, among others.

> **"Does the government know why many fishermen engage in illegal fishing despite the efforts to end the menace?**

rasi exchange of fire

Scanned with CamScanner



BIASHARA

MWANANCHI UK 21

# Minofu ya samaki yasafirishwa

**Jesse Mikofu,** Mwananchi
jmikofu@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Kilichokuwa kinasubiriwa kwa muda mrefu na wafanyabiashara wa mizigo na wakazi wa jijini Mwanza sasa kimetimia baada ya ndege ya mizigo kuanza kusafirisha minofu ya samaki kutoka jijini hapo kwenda Ulaya.

Waziri wa ujenzi, uchukuzi na mawasiliano, Isack Kamwelwe alieleza hayo jana wakati akipokea injini mbili kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya katika bandari ya Mwanza Kusini.

Alisema ndege hiyo imeanza rasmi kusafirisha shehena ya minofu hiyo kutoka Mwanza kwenda moja kwa moja hadi Amstadarm, Uholanzi.

Alisema ndege hiyo imesafirisha tani nane za minofu ya samaki na inatarajiwa kurejea Mwanza Alhamisi ijayo kusafirisha shehena nyingine ya mizigo.

"Leo (jana) kuna matukio mawili makubwa, kwanza nawataarifu kwamba Mwanza sasa uwanja wake umekuwa wa kimataifa rasmi kuanzia leo, kuna ndege imeondoka na minofu ya samaki kwenda Amstadam," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wakuu wa mikoa ya Mwanza, Geita, Kagera na Mara inayozungukwa na ziwa Victoria kutengeneza umoja na kukusanya samaki kwa pamoja, ili wawe wanachukuliwa kutoka Mwanza.

Alisema kwa sasa Serikali inafanya utaratibu ili iwe na ndege kwa ajili ya kubeba mizigo kuitoa hapa nchini kuipeleka nchi za Ulaya.

Kuhusu ujenzi wa meli mpya, waziri huyo aliwataka wakandarasi kuhakikisha unakamilika mapema kulingana na mkataba.

Naye mtendaji mkuu wa kampuni ya huduma za meli, Eric Hamis alisema kwa sasa ujenzi wa meli hiyo umefikia asilimia 65.

Meli hiyo inayogharimu Sh89.7 milioni ilianza kutengenezwa Januari mwaka jana na inatarajiwa kukamilika Januari 2021.

Scanned with CamScanner



UHURU

# Kilo 28,450 za samaki zagawiwa kwa yatima

BUNGE limeelezwa kuwa jumla ya kilo 28,450 za samaki wachanga zilizokamatwa kwenye operesheni mbalimbali za kudhibiti uvuvi haramu, zimegawiwa katika vituo vya kulelela watoto yatima pamoja na wananchi wenye mahitaji maalum.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliyaeleza hayo jana, Bungeni, kufuatia swali lililoulizwa na Mbunge wa Viti Maalumu (Chadema), Aida Khanani.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji kwanini wavuvi wengi wanatumia nyavu haramu wakati serikali inafahamu suala hilo.

Ikijibu swali hilo, wizara hiyo ilisema inafahamu baadhi ya sababu zinazowafanya wavuvi kutumia nyavu haramu.

Ilibainisha kuwa miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na ukosefu wa elimu na uelewa kwa baadhi ya wavuvi kuhusu madhara ya uvuvi huo.

Aidha, ilifafanua kuwa tabia za ubinafsi uliokithiri na tamaa kwa baadhi ya wavuvi ya kupata utajiri kwa muda mfupi bila kujali madhara yanayotokea kwenye rasilimali za uvuvi, mazingira na afya za walaji.

"Kutokana na hali hiyo, vitendo vya uvuvi haramu vimeendelea kuongezeka siku hadi siku, hali inayoweza kusababisha kupungua au kutoweka kwa rasilimali za uvuvi iwapo hatua za udhibiti zisingechukuliwa.

"Katika kubaliana na vitendo vya uvuvi haramu, serikali imeendelea kuielimisha jamii kuhusu njia za uvuvi endelevu na madhara ya uvuvi haramu,"ilieleza.

Wizara hiyo ilieleza kuwa elimu hiyo imekuwa ikitolewa kwa njia mbalimbali, ikiwemo redio, runinga, semina na maonesho mbalimbali, yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Siku ya Chakula Duniani.

"Katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu, wizara imeendesha vipindi 19, vya redio na vipindi 34, vya runinga na makala mbalimbali kuhusu uvuvi endelevu, ufugaji bora wa viumbe kwenye maji na uhifadhi wa mazingira.

"Vilevile, katika kipindi hicho, jumla ya wananchi 43,104, waliemishwa kuhusu uvuvi endelevu, ufugaji bora wa viumbe kwenye maji na uhifadhi wa mazingira kupitia mafunzo rejea pamoja na maonesho ya Sabasaba na Nanenane," ilieleza.

Aidha, ilibainisha kuwa imeendelea kuendesha doria na operesheni mbalimbali ili kudhibiti uvuvi haramu, ambapo zana mbalimbali za uvuvi haramu na vifaa vinavyosaidia uvuvi haramu vilikamatwa.

Ilivitaja vifaa hivyo ni zana na vifaa vilivyokamatwa kwa kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu, ni pamoja na nyavu za kokoro 808, Kamba za kokoro zenye urefu wa mita 149,071, nyavu za makila 15,911 na zenye macho chini ya inchi sita kwa uvuvi wa Ziwa Victoria.

Zana zingine ni nyavu za makila 3,754, zilizounganishwa kwa kina, nyavu za makila 600, zenye macho chini ya inchi tatu kwa uvuvi wa maji mengine, nyavu za timba 2,571, nyavu za ringnet 204, zenye macho chini ya milimita nane, nyavu za kumbakumba au gizagiza 117.

Vyavu zingine zilizokamatwa ni nyavu za dagaa 493, zenye macho chini ya milimita nane, vyandarua 22, ndoano 10,601, boti 72, mitumbwi 680, injini za boti 275, magari 8 na pikipiki 27.

Aidha, ilisema jumla ya kilo 28,450 za samaki wachanga zilikamatwa na kugawiwa katika vituo vya kulelela watoto yatima pamoja na wananchi wenye mahitaji maalum.

kubwa serikali inawajali wananchi wake wote bila kujali kiwango cha kipato anachokipata

kukopa kutoka Benki Kuu kwa unafuu zaidi kuliko ilivyokuwa awali," alisisitiza kwenye

wananchi kuchukua hatua na tahadhari dhidi ya kuenea kwa virusi vya corona nchini.

kufanya
ibu wa
alisema.
siasi si
a.
na haki
wajibu

atimua
lakini
kufuata
ingi ya
eria za
nchi na

Ndugai,
adema,
nuli za
a taifa,
iwe na

dhi ya
watisha
nyakati
kurudi
anataka

## UTEKELEZAJI




WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (wa pili kushoto), akimkabidhi injini ya boti Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia, kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ushirika wa wavuvi jimboni humo, jana. Jumla ya injini 13 zenye thamani ya sh. milioni 60 zilizotolewa bure na Wizara hiyo kusaidia wavuvi katika Maziwa, Mito, Mabwawa na Bahari. (Picha na Wizara ya Mifugo).

Scanned with CamScanner

Waziri Mpina alisema injini nyingine 60 zenye thamani ya Sh. milioni 260 zi-

Rais John Magufuli alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hivyo kumshukuru

leta matokeo chanya yaliyotarajiwa na serikali.

NIPASHE UK 19



Fundi Said Mwandike, akitengeneza vyombo vya kulishia mifugo kwa ajili ya kuuza ili ajipatie riziki, katika Soko la Vetenari, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wajawazito wawekewa utaratibu

tali kwa shughuli za ... kupunguza msongamano benki. Benki pia wanashauriwa kuhamasisha wateja kuongeza matumizi ya mifumo ya malipo ya dijitali kwa shughuli za uwekaji na utoaji fedha," ilisema.

Ilisema BoT inaendelea kuangalia

... zi nchini zinapaswa kufanywa kwa shilingi na BoT inaendelea kushauri umma kuchukua hatua za kupunguza kuenea kwa Covid-19 nchini.

MTANZANIA UK 4

# Samaki wa Ziwa Victoria sasa kuuzwa moja kwa moja Uholanzi

**Na BENJAMIN MASESE**
-MWANZA

SERIKALI imepokea injini mbili kutoka Korea Kusini ambazo zitafungwa kwenye meli mpya ya MV Mwanza, huku ikizindua pia safari za ndege kusafirikisha minofu ya samaki kwenda nchini Uholanzi ambapo Shirika la ndege la Rwanda litakuwa likiisafirisha.

Mbali na kuzindua usafirishaji huo wa samaki, pia imetangaza kwamba sasa uwanja wa ndege wa Mwanza unakuwa wa kimataifa.

**Meli**

Akizungumza jijini Mwanza jana baada ya kuzindua safari za ndege na kupokea injini hizo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Isaack Kamwelwe, meli inayotengenezea jijini Mwanza itakuwa ikifanya za Mwanza-Bukoba na nchi jirani za Kenya na Uganda

Alisema meli hiyo inayogharimu Sh bilioni 159 inatarajia kukamilika na Januari 2021 na kuwataka wakandarasi ambao ni Gas Entec Co. Ltd, Kangnam Corporation zote kutoka Korea ya Kusini zikishirikiana na Suma JKT ya Tanzania kuhakikisha zinakamilisha shughuli hiyo kama mkataba unavyoelekeza.

"Meli hii itakuwa kubwa kuliko meli zote katika ukanda huu wa maziwa makuu, itakuwa na mita 92.6, kimo chake kitakuwa mita 11.2, upana mita 17 na uzito wa tani 3,500 kwa takwimu hizo ndio itakuwa meli kubwa kuliko zote na itakuwa inatumia masaa saba kutoka Mwanza hadi Bukoba,"alisema.

Akitoa ufafanuzi wa injini hizo, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania (MSCL), Erick Hamisi, alisema injini hizo zimenunuliwa kwa Dola za Marekani 39,000,000 sawa na Sh bilioni 89.764 na kila moja ina tani 35 na uwezo wa kuzaliza KW 2,380. Alisema uwezo huo wa injini utaiwezesha meli hiyo kusafiri kwa saa sita kutoka Mwanza hadi Bukoba na kwamba hadi sasa wakandarasi hao wamelipwa Sh bilioni 55.618 sawa na asilimia 64 ya gharama zote.

**Safari za ndege**

Katika hatua nyingine Kamwelwe alizindua safari za Mwanza hadi hadi Uholanzi katika kwa kutumia shirika la Ndege ya Rwanda ambapo jana ilisafirishwa tani nane za minofu ya samaki huku akifafanua kwamba kila wiki kutakuwa na safari moja.

Kutokana na safari hizo, amewaagiza wakuu wa mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu na Kagera kuunda mtandao wa pamoja wa kuhakikisha samaki wote wanaletwa kwenye viwanda ili kurahisisha upatikanaji wa minofu hiyo na kufikishwa uwanja wa kimataifa wa Mwanza.

Scanned with CamScanner

ya Tarime.

NYANGA

## ...ambi akosa ...mana

...IAN MASYENENE

...a uhujumu uchumi in-
...bili Mbunge wa Kishapu
Shinyanga (CCM), Sulei-
...soud (Nchambi), imetajwa
...a Mahakama ya Hakimu
...Wilaya ya Shinyanga, huku
...wa mshtakiwa ukishindwa
...sha maombi yake ya dha-

...mbi alipandishwa kizim-
...a mara ya kwanza Mei 8,
... huu mahakamani hapo
...hauri namba 10 la mwaka
...kusomewa mashtaka 12 ya
... uchumi mbele ya Hakimu
...wandamizi, Ushindi Swalo.
...takiwa aliingia viwanja vya
...ma saa 3:47 asubuhi, huku
...lake likionekana kuvuta
...wengi na kuhudhuriwa na
...balimbali, wakiwemo wa-
...madiwani, wananchi na fa-
... mbunge huyo ambao wal-
...nje ya chumba (chemba)
...kimu Mkazi Mwandamizi,
... Swalo lilikokuwa likiende-
...ri hilo.
...nde wa mshtakiwa, ukion-
...na Wakili Frank Mwalongo
... mteja wao apate dhamana,
...maombi yao yalishindikana
...ya upande wa mashtaka
...zwa na Mkuu wa Mashtaka
...wa Shinyanga, Margareth
...a kupinga na kueleza kuwa
...ma hiyo haina uwezo wa
...hamana.Hakimu Swalo ali-
...na na hoja hiyo na kuahiri-
...uri hilo hadi Mei 25, mwaka

TARIME

MTANZANIA UK 8

# *Wananchi walalamikia Jeshi la Polisi kuwaachia wezi wa mifugo *

**Na PETER FABIAN**

WANANCHI na viongozi wa Serikali za vijiji vya kata za Wilaya ya Rorya vinavyopakana na maeneo ya Wilaya ya Tarime kwa pamoja, wamelalamikia baadhi ya maofisa wa polisi Kanda Maalumu ya Tarime/Rorya kuwachia wezi wa mifugo wanaokamatwa na wananchi na kufikishwa katika vituo vya Polisi wakiwa na mifugo waliyoiba.

Viongozi wa vijiji na watendaji wa kata hizo, wakizungumza wakati wa kikao cha ndani na Mbunge wa Rorya, Lameck Airo (CCM) kilichofanyika Kijiji cha Sakawa jana na kumweleza jinsi wizi wa mifugo ulivyoibuka kwa kasi na kuwa kero.

Wizi huo, unafanyika kata za Ikoma, Goribe, Kitembe, Mirare, Kirogo, Kigunga,Mkoma na Bukwe za Wilaya ya Rorya.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyamasanda,John Midega alimweleza Airo kilio cha wananchi na wafugaji walivyoathiliwa zaidi na wizi wa mifugo hali inayosababusha kushindwa kujishughulisha na shughuli za kilimo na maendeleo kutokana na kila kukicha kufatilia nyayo za mifugo inayoibiwa nyakati za jioni na usiku kwenye maboma ya kulaza mifugo.

"Wananchi wamekuwa wakishirikiana na viongozi wa serikali za vijiji na watendaji wa vijiji na kata kufatilia nyayo za mifugo iliyoibiwa, wanapobahatika kukamata wezi na kuwafikisha vituo vya polisi vya Shirati, Utegi na Sirari, watuhumiwa wamekuwa wakiachiwa na kurudi kuwatishia wananchi, kuwavamia usiku na kuwajeruhi kwa mishale na mapanga,"alisema.

Diwani wa Kata ya Ikoma, Andrew Nyakriga alisema hali ni mbaya na wananchi wameingiwa woga kutokana na kushamiri kwa matukio ya wizi wa mifugo.

"Haiwezekani polisi kazi iwe kuwageuzia kibao na kuwakamata wananchi wanaowafikisha wezi katika vituo vya wilaya za kipolisi vya Shirati, Utegi (Rorya) na Sirari (Tarime) Kanda Maalumu na maafisa wake kuwaachia wezi na kuwageuzia wananchi na kuwafungulia kesi ikiwa ni pamoja na kuwatisha wasiendelee kufatilia kesi za watuhumiwa wa matukio ya wizi,"alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyabirongo, Jastine Chandi alikiri kijiji chake na vingine jirani vya Matamankwe, Nchoke, Bumera, Kubiterere na Sirari kudaiwa kuwa maficho ya mifugo inayoibiwa Wilaya ya Rorya.

Naye Airo aliwahakikishia viongozi hao na watendaji kulifikisha suala la wizi lililoibuka upya kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), pia waziri husika.

Airo alisikitishwa na taarifa za kutajwa kwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Kanda Maalumu Tarime/Rorya, Denis Mnjumba Mkuu wa Polisi Kituo cha Sirari, Utegi na OC- CID Kituo cha Shirati kuwakumbatia na kuwalinda wezi ambao wamekuwa wakiwaachia na kuwabadilishia kibao wananchi na viongozi wanaopambana kudhibiti wizi wa mifugo kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Saimon Chacha alikiri kuibuka kwa kasi wizi mifugo na kudai kuwa matukio ya wizi wa ng'ombe wawili hadi sita yamekuwa ya kawaida kwa siku za hivi karibuni.

sasa...
kuny...
kuha...
wan...
na k...
nyin...
kwa...
mais...
kupe...
B...
la tu...
hiyo...
wa s...
mmo...
lake...
zipo...
na ku...
famil...
hayo...
madh...
hayo...
M...
Nyaka...
Maha...
usiku...
alipat...
imean...
tukio...
wake...
Al...
kwa n...
famili...
hospit...
Nyash...
walipe...
rufaa...
walifa...
wanap...
Ali...
za mta...
kwa m...
siyo in...
wanan...
hayo n...
salama...
wao wa...

MASWA

# Wananchi zaidi ya 3,000 wapata tumaini ji...

Scanned with CamScanner

...e thamani ya sh. bilioni 217.5

UHURU UK 3

## ... kwa njaa *

...sukari nchini umetokana na baadhi
...abiashara kuficha bidhaa hiyo na
...gonjwa wa covid-19, kusababisha
...agizwa nje ya nchi kuchelewa

...gumza jana, Bungeni, Hasunga
...tika kukabiliana na upungufu wa
...ikali ilitoa kibali cha kuingiza tani
...oka nje ya nchi, Machi, mwaka huu.
... cha pamoja na wawakilishi wa
... serikali, Mamlaka ya Mapato
...TRA) na Bodi ya Sukari chini ya
...u (Kassim Majaliwa), tulikubaliana
...ri haitapanda maana gharama za
...ilikuwa zipo chini.
... hivyo, kumejitokeza kuchelewa
...hini kutokana na ugonjwa wa
...baadhi ya wanunuzi kuficha sukari,
...i tatizo," alieleza.
...huyo alisema wizara kupitia bodi ya
...nya uchunguzi wa kina kwa kutumia
...asnia ya sukari, ambapo ilichukua
...utangaza bei elekezi ya jumla na
...tika mikoa yote ya Tanzania Bara,
...la kukabiliana na wafanyabiashara
...ninifu.
... hivi ni kweli katika maeneo
...i kuna upungufu wa sukari, ni
...a meli nyingi zimekuwa 'zikifaulisha'
...eli nyingine, hivyo mzigo hauji kadri
...wa," alisema.
...eza:"Tani zilizowasili na zilizowasili
...nyingine zikiwa zimetolewa ni tani
...zopo njiani ni tani 21,000, zote
...wezi huu."
...za, alisema tani 500, zilizotoka Afrika
...neshafika, hivyo hakutegemewi
...pungufu wa sukari kwani mahitaji
... 35, kwa mwezi na iliyoingizwa ni
...
...da vilikuwa vianze uzalishaji
...honi, lakini kutokana na mvua
... kunyesha ni kiwanda kimoja
...onyesha dalili ya kuanza uzalishaji
... mwezi.
...kikishie Watanzania kuwa, kwa
...ingia na hatua zilizochukuliwa,
...osha kabisa na hatuhitaji kuwa
...ufu wa sukari. Wanaohusika
... sukari iliyofika wanaiotoa na
... usambazaji katika mikoa yote
...eza.
...huyo alisema serikali imekokotoa
...i inayotoka nje mpaka inafika Dar
...i dola 350 na ile inayotoka Brazil
... Kwa sababu hiyo, alisema bei ya
...i haitakiwi kuzidi kwa bei elekezi
...a



...Kampuni ya GBP, mjini Tanga,

## Mabilioni sekta uvuvi yaongeza imani kwa wadau bajeti mpya *

**Na MWANDISHI WETU**

**WAKATI** Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikitarajiwa kuwasilisha makadirio yake ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, wadau wa uvuvi wametaka sekta hiyo kuwekewa kipaumbele ili kuongeza kasi zaidi ya mafanikio, ikiwamo pato litokanalo na mauzo ya samaki.

Tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, imefanikiwa kuongeza udhibiti katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na sekta ya uvuvi, ikiwamo kufanya operesheni dhidi ya uvuvi haramu.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na mauzo ya nje, yakiongezeka kutoka sh. bilioni 379 hadi sh. sh. bilioni 680.

Akizungumza na gazeti la Uhuru, kuelekea kusomwa kwa bajeti ya wizara hiyo, Nyamagori Bujura, mfanyabiashara wa biashara ya samaki katika mikoa ya Mwanza na Mara, alisema kwa sasa kila mmoja anashuhudia ongezeko la samaki na hata mapato yatokanayo na uvuvi, jambo ambalo linapaswa kuendelezwa.

"Awali, wakati kulipokuwa kukifanyika operesheni mbalimbali dhidi ya uvuvi haramu, nilikuwa naona kama vile serikali inakuja kutuharibia maisha, lakini kwa ninanchokishuhudia sasa, kutokana na ongezeko la samaki, nathubutu kusema bajeti ijayo itenge fungu la kutosha kusimamia uvuvi salama na wenye tija, kwa kuwa unatusaidia hata sisi kupata samaki wengi na wakubwa," alisema.

> **"Wakulima nendeni mkalime, wafugaji nendeni mkafuge, wavuvi nendeni mkavue, serikali iko pamoja nanyi kulinda soko la ndani na Waziri Mkuu, tumeshakataa kukatishwa tamaa na mtu ...**
>
> Waziri Mpina.

Kwa upande wake, Habibu Jokolowela, mkazi wa Ukerewe, alisema wavuvi wana imani kubwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kwamba, wanachotarajia katika bajeti mpya ni wizara hiyo kuongezewa uwezo wa kushirikiana na wavuvi ili kupata mafanikio zaidi.

Kauli za wadau hao zinakuja wakati serikali ikiwa imechukua hatua mbalimbali katika kuendeleza sekta ya uvuvi kwa miaka mitano iliyopita na kufanikiwa kuongeza pato litokanalo na sekta hiyo.

Akizungumza katika hafla ya ufungaji wa maonyesho ya wakulima, yaliyofanyika mjini Bariadi, mkoani Simiyu, Agosti 2019, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alimhakikishia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo kwamba, wizara yake itaendelea kusimamia kikamilifu ulinzi wa rasilimali za mifugo na uvuvi na kuwahakikishia wafugaji na wavuvi soko la ndani la bidhaa zao halitachezewa tena.

"Wakulima nendeni mkalime,

Inaendelea UK. 20

Scanned with CamScanner

uk19.

# *Waziri akabidhi injini za* mil. 320/- kwa wavuvi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amekabidhi injini 73 za boti za uvuvi zenye thamani ya Sh. milioni 320 kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ushirika wa wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akikabidhi injini hizo kwa Wabunge Makao Makuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mtumba mjini Dodoma, Waziri Mpina alisema kati ya injini hizo 73 serikali imegawa bure injini 13 zenye thamani ya Sh. milioni 60 kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ushirika wa wavuvi.

Waziri Mpina alisema injini nyingine 60 zenye thamani ya Sh. milioni 260 zimetolewa kwa ruzuku ya serikali ambapo wavuvi wamechangia asilimia 60 na serikali imechangia asilimia 40 kama sehemu ya kuwezesha ukuaji wa sekta ya uvuvi.

Wakizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mbunge wa Kyela na Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alimshukuru Mpina kwa kuamua kuwasaidia wavuvi vifaa vya kisasa vya kuvulia na kwamba vitaleta tija kubwa kwa wavuvi wa Ziwa Nyasa.

Naye Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia, alisema msaada wa serikali kwa wavuvi mara ya mwisho ulitolewa wakati Rais John Magufuli alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hivyo kumshukuru Waziri Mpina kwa uamuzi huo wa kuwakumbuka na kuwasaidia zana za kisasa wavuvi.

Mbunge wa Ukerewe, Joseph Mkundi, alisema msaada huo umekuwa wakati mwafaka na kuonyesha serikali inathamini maendeleo ya uvuvi tofauti na dhana iliyojengeka hapo awali kwamba serikali kazi yake ni kukamata tu wavuvi kwa zana haramu.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, alisema msaada huo utakuwa chachu ya mabadiliko ya wavuvi katika Wilaya ya Kaliua, na kwamba wilaya hiyo itahakikisha vifaa hivyo vinatunzwa ili viweze kuleta matokeo chanya yaliyotarajiwa na serikali.

Scanned with CamScanner